**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**BODI YA PAMBA TANZANIA**

# Kanuni 10 za Kilimo Bora cha Pamba



## UTANGULIZI

Pamba ni zao muhimu la kimkakati na biashara nchini, linachangia takriban asilimia kati ya 10 na 20 ya pato la taifa la fedha za kigeni, linatoa ajira kwa karibu asilimia 40 ya Watanzania wote walio ndani ya mnyororo wa thamani na chanzo cha malighafi kwa viwanda vya nyuzi, nguo na mafuta. Uzalishaji wa pamba hutekelezwa Kanda ya Magharibi na Kanda ya Mashariki. Pamba kwa Kanda ya Magharibi huzalishwa katika mikoa kumi na mbili (12) ambayo ni Simiyu, Shinyanga, Geita, Mwanza, Tabora, Mara, Kagera, Katavi, Kigoma, Singida, Manyara na Dodoma na uzalishaji ni zaidi ya asilimia 98.Aidha pamba huzalishwa Kanda ya Mashariki katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Iringa, Kilimanjaro na Tanga ambapo uzalishaji ni chini ya asilimia 2. Ili kuongeza tija na ubora wa pamba, mkulima anatakiwa kuzingatia kanuni za kilimo bora cha Pamba kama ifuatavyo;


## 1. TAYARISHA SHAMBA MAPEMA

Shamba la kupanda pamba ni muhimu litayarishwe mapema , mwezi mmoja kabla ya kuanza kwa msimu wa kupanda. Matayarisho haya ni pamoja na kufyeka, kung'oa visiki, kukatua, kuweka mbolea ya samadi, kupiga haro na kuweka matuta

**Faida za kutayarisha shamba mapema**

Kutoa muda wa kutosha kwa majani na takataka nyingine kuoza na kuchanganyika na udongo na kuwa chakula cha mimea itakayopandwa. Kusaidia maji kupenya ardhini kwa urahisi na kuhifadhi kiasi cha kutosha kwa ajili ya mbegu zitakazopandwa Kumwezesha mkulima kupanda mara tu mvua zinapoanza kunyesha.





Maandalizi ya shamba kutumia trekta Kuandaa shamba kwa jembe la mkono

## 2. TUMIA MBOLEA ZA SAMADI NA VIRUTUBISHO VINGINE

Ardhi inapotumika kwa muda mrefu hupoteza rutuba yake ya asili na uwezo wa kutoa mavuno mengi na yaliyo bora. Mkulima unashauriwa kuongeza mbolea ya samadi shambani kila msimu. Ongeza tani 7.5 hadi 10 kwa hekta na tani 3 hadi 4 kwa ekari. Au weka viganja viwili (2) katika kila Shimo wakti wa kupanda mbegu. Vilevile mkulima anaweza kutumia mbolea ya viwandani kupandia kiasi kati mbolea na mbegu kabla ya kufukia

**Faida za kutumia mbolea ya samadi**

. Ina viini lishe vinavyohitajiwa na mmea

. Ina uwezo wa kuhifadhi na kurutubisha udongo kwa muda mrefu

. Inaimarisha uwezo wa udongo kuhifadi maji kwa muda mrefu

. Kuongezeka kwa Mavuno ya mkulima





### 3. PANDA PAMBA MAPEMA

Pamba ipandwe mapema mara mvua zinapoanza kunyesha au kukaribia kunyesha. Pamba ikipandwa mapema itakua na kukomaa vizuri na hivyo kupata mavuno bora na mengi.

Kwa mikoa ya kanda ya Magharibi pamba ipandwe kati ya tarehe 15 Novemba na 15 Desemba na kwa upande wa Kanda ya Mashariki mkulima panda pamba kati ya 15 Februari hadi 15 Machi

### 4. PANDA KWA MISTARI NA KWA NAFASI MAALUM.

Matuta ya futi tatu au sesa

Kama shamba limepigwa matuta ya futi tatu (sentimita 90) na lina rutuba ya kutosha panda mstari mmoja tu juu ya tuta , nafasi kati ya shimo na shimo (mche na mche) iwe sentimita 30 au futi moja na nafasi kati ya mstari na mstari ni sentimita 60. Kwenye shamba lisilo na matuta yaani sesa, panda pamba kwa nafasi ya sentimita 60 au futi mbili kutoka mstari hadi mstari na sentimita 30 au futi moja kutoka shimo hadi shimo.

Faida za kupanda kwa mistari

kurahisisha kazi ya palizi na unyunyiziaji wa viuadudu.

inakuhakikishia kuwa na mimea ya kutosha kwa eneo

am bayo ni mimea 44,444 kwa ekari au mimea 111,110 kwa hekta.

. kupunguza matumizi makubwa ya mbegu yasi yokuwa ya lazima.

**5. PANDA IDADI HALISI YA MBEGU KATIKA KILA SHIMO.**

Panda mbegu tano (5) tu katika kila shimo kama mbegu zina mabaki ya nyuzi au mbegu tatu (3) iwapo mbegu zimeondolewa nyuzi. Iwapo utapanda kwa idadi ya mbegu kama inavyotakiwa, kilo 20 au debe mbili za mbegu zenye mabaki ya nyuzi zinatosha kupanda ekari moja na kilo kumi (10) za mbegu iliyondolewa nyuzi inatosha kupanda ekari moja. Athari za kupanda mbegu nyingi ni pamoja na;-

Miche ya pamba kubanana na kudhoofika

Kutumia mbegu nyingi na hivyo kuongeza gharama za uzalishaji

## 6. PUNGUZA MICHE

Majuma manne tangu pamba ipandwe na kuota, miche ya pamba ipunguzwe na kubakiza miwili tu iliyonawiri na yenye afya katika kila shimo. Mkulima akichelewa kupunguza miche iliyozidi shambani, pamba itachelewa kutoa matawi na maua. Miche mingi shambani haina tofauti na magugu kwa sababu hushindania chakula na virutubisho vingine na kufanya pamba yote idhoofike.

UPUNGUZIAJI



7.0 PALIZI KWA WAKATI

Shamba la pamba lipaliliwe mapema mara magugu yanapoanza kuota. Palizi ya kwanza ifanyike si chini ya mwezi mmoja tangu pamba kuota. Ukichelewa kupalilia pamba itashambuliwa na magugu na hivyo kuathiri kiasi cha mavuno kitakachopatika kwa takriban asilimia 50 au zaidi



.

PALIZI KWA JEMBE LA WANYAMAKAZI



Palizi kwa jembe la mkono

## 8. KUNYUNYIZIA VIUADUDU KUZUIA WADUDU WAHARIBIFU

Kuna visumbufu vingi ambavyo hushambulia zao la pamba kwa kutafuna na kufyonza vitumba/majani, baadhi ya wadudu waharibifu wa pamba ni pamoja na funza wa vitumba, kangambili, vidukari, funza mwenye nywele , chawajani na kaledea. Wadudu hawa wakiachwa bila kudhibitiwa wanaweza kuleta hasara ya zaidi ya nusu ya mavuno yote ambayo yangepatikana. Hivyo ni muhimu kunyunyizia madawa ya kuwaangamiza mara tu mmea wa pamba unapoanza kuonyesha dalili za mashambulizi au uwepo wa wadudu waharibifu



Wadudu wafyonzao



Wadudu wafyonzao

**Athari za kutonyunyizia**

Kushuka kwa ubora wa pamba kutokana na pamba nyingi kuwa fifi au daraja B.

Kupungua kwa mavuno kwa zaidi ya asilimia 80





9. **VUNA PAMBA MAPEMA NA CHAMBUA**

Vuna mapema pamba iliyokomaa na kupasuka vizuri nakuichambua sawasawa. Ukichelewa kuvuna pamba itaharibiwa na vumbi, mvua,



takataka au wanyama na hivyo kuharibu usafi na ubora wake na kumkosesha mkulima kipato. Aidha baada ya kuvuna pamba ichambue na uitenge katika madaraja ya A na B kabla ya kwenda kuuza.

Pamba daraja A ni pamba iliyokomaa vizuri, nyeupe na isiyo na uchafu au takataka zozote na huuzwa kwa bei kubwa kuliko pamba daraja B.

**10 NG'OA NA KUCHOMA MOTO MASALIA YOTE YA PAMBA**

Mara tu baada ya kuvuna pamba, ng'oa na kuchoma moto masalia na takataka zote za pamba kabla ya tarehe 15 septemba ili kupunguza au kudhibiti mzunguko wa wadudu waharibifu wa pamba na vimelea vya magonjwa. Kwa kufanya hivi utakuwa umepunguza ongezeko la wadudu ambao wangeweza kuzaliana kwenye masalia hayo na hivyo kupunguza masambulizi ya wadudu msimu unaofuata. Iwapo mkulima

atazingatia kanuni hizi kwa ufasaha, ataweza kujipatia mavuno ya kati ya kilo 800 na 1800 za pamba kwa ekari. Kwa ushauri zaidi muone A sa Ugani aliye karibu nawe

**Miti/masalia ya pamba yanaweza kutumika kama nishati mbadala (KUNI)**



## KALENDA YA KILIMO CHA PAMBA – KANDA YA MAGHARIBI

| KANUNI/SHUGHULI | | MIEZI | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | JAN | FEB | MACHI | APR. | MEI. | JUNI | JULAI | AGOSTI | SEPT. | OCT. | NOV. | DES. |
| 1 | Kutayarisha Shamba mapema | | | | | | | | | | | | |
| 2 | Kurutubisha ardhi/Kuweka Samadi | | | | | | | | | | | | |
| 3 | Kupanda Pamba Mapema | | | | | | | | | | | | |
| 4 | Panda idadi ya Mbegu Inayopendekezwa | | | | | | | | | | | | |
| 5 | Kupanda Pamba kwa Mistari na Nafasi Maalum | | | | | | | | | | | | |
| 6 | Punguzia Miche (Ibaki miche miwili kila shimo) | | | | | | | | | | | | |
| 7 | Palilia kwa wakati na Mara kwa Mara | | | | | | | | | | | | |
| 8 | Nyunyizia Viuadudu | | | | | | | | | | | | |
| 9 | Vuna pamba mapema,Tenga katika madaraja na kuuza | | | | | | | | | | | | |
| 10 | Ngoa na Choma Masalia ya Pamba | | | | | | | | | | | | |

## KALENDA YA KILIMO CHA PAMBA KANDA YA MASHARIKI

| KANUNI/SHUGHULI | | MIEZI | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | JAN | FEB | MACHI | APR. | MEI. | JUNI | JULAI | AGOSTI | SEPT. | OCT. | NOV. | DES. |
| 1 | Kutayarisha Shamba mapema | | | | | | | | | | | | |
| 2 | Kurutubisha ardhi/Kuweka Samadi | | | | | | | | | | | | |
| 3 | Kupanda Pamba Mapema | | | | | | | | | | | | |
| 4 | Panda idadi ya Mbegu Inayopendekezwa | | | | | | | | | | | | |
| 5 | Kupanda Pamba kwa Mistari na Nafasi Maalum | | | | | | | | | | | | |
| 6 | Punguzia Miche (Ibaki miche miwili kila shimo) | | | | | | | | | | | | |
| 7 | Palilia kwa wakati na Mara kwa Mara | | | | | | | | | | | | |
| 8 | Nyunyizia Viuadudu | | | | | | | | | | | | |
| 9 | Vuna pamba mapema,Tenga katika madaraja na kuuza | | | | | | | | | | | | |
| 10 | Ngoa na Choma Masalia ya Pamba | | | | | | | | | | | | |